



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

Kumb. Na.HWB/I.20/49/173.

TANGAZO

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WA HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO KUHUSU, KUFUNGULIWA RASMI KWA DIRISHA LA UTOAJI WA MIKOPO YA 10% KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU

HALMASHAURI IMETENGA JUMLA YA THS 1,037,367,233.81 KWA AJILI YA UTOAJI WA MIKOPO HIYO

MKURUGENZI MTENDAJI ANAWATANGAZIA WANAVIKUNDI WOTE WENYE SIFA KUTUMA MAOMBI YA MKOPO KUPITIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA WEZESHA PORTAL KUANZIA TAREHE 23.09.2024 HADI TAREHE 22.10.2024

Shauri Selenda

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, Barabara ya Uhindini, S.L.P. 59, 61301 BAGAMOYO Mkoa wa Pwar
Simu Na: 0733 860 575, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: ded.bagamoyo@pwani.go.tz. Tovuti: www.bagamoyodc.go.tz



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

Kumb. Na.HWB/I.20/49/173.

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE,
VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1))

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ambapo jumla ya Shilingi **1,037,367,233.81** zimetengwa katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025 Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za serikali za mitaa zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- (i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na halmashauri,
- (ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,
- (iii) Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya menejimenti ya halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,
- (iv) Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kijasiriamali; na
- (v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Barua zote ziadikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, Barabara ya Uhindini, S.L.P. 59, 61301 BAGAMOYO Mkoa wa Pw
Simu Na: 0733 860 575, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: ded.bagamoyo@pwani.go.tz Tovuti: www.bagamoyodc.go.tz

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na afisa maendeleo ya jamii wa Kata husika au mtendaji wa Kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo; barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na afisa mtendaji wa kijiji/mtaa, muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo na taarifa ya akaunti ya benki.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 22, mwezi 10, mwaka 2024

Tangazo hili limetolewa na: -

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, Barabara ya Uhindini, S.L.P. 59, 61301 BAGAMOYO Mkoa wa Pwani
Simu Na: 0733 860 575, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: ded.bagamoyo@pwani.go.tz Tovuti: www.bagamoyodc.go.tz